Petero alikua afanyike mvuvi wa watu lakini mtandao wa kale haungefanya
kazi katika hali ya kiroho, basi ingebindi neti hiyo ipasuke kama ilivyo sasa
mitandao ya kindini haiwezi kufanya kazi ya kiroho maana kama ingekua
sasa, Wayahundi wangemtambua Yesu kuwa ni Mesia. Petero ilimbindi aondoke katika mtandao uliokuwa wa kale na kuingia katika mtandao wa
kisasa ili awapate watu wote katika hali ya kuondoa pengo katikati ya wayahudi na wayunani.
Lazima nyavu aliokuu ipate kuvunjika ili njavu mpya ifanye kazi.
Yesu hakunja kuondoa sheria lakini alikunja kuifanya iwe na maana mpya
kwetu.
Yeye hakuondoa habari za kafara ya dhabi kupitia ndamu ya wanyama lakini
aliikamilisha kwa ndamu yake. Yesu alionya kuhusu ndivai mpya kuiweka
katika mfuko uliowakale, maana alinjua kwamba mifuko mifuko iliyozeeka
haiwezi kubeba ndivai mpya, hali kadhalika nyavu za kitambo haziwezi kuvua
samaki wa kisasa.Habari njema Ya Ufalme haiwezi kuenezwa na net za kitambo. Kakati ya habari ya nyavu za kwanza zilizo vunjika basi kul;iundwa
neti mpya, na hali hii ya kiasili inatuonyesha yanyotendeka katika roho..

**NIRA**

Nira zilitumika katika ulimwengu wote katika hali ya kufunga wanyama pamoja ilikufanya kazi katika shamba wakati wa mavuno. Yesu alinena kuhusu nira akisema;

**Njooni kwangu enyi mlioshoka na kubebeshwa mizigo mizito, na nitawapumzisha,**
**Njituike nira yangu, na unjifunze name, maana mimi ni mpole na…..**
**maana nira yangu ni rahisi na mzigo wangu mwepesi….. (Matthew 11:28-30)**

Maono alioyapeana ni ya mavuno, leo shamba hilo la mavuno linamaanisha
watu bilioni tatu. Ambao hawanjawahi kupokea Injili hii…. Na anatupa shangamoto hii… ni lahisi na nyepesi. Hivyo ndivyo anavyomaanisha kwamba hali ya kuvuna ni lahisi na nyepesi kama ukitumia binu za kiroho.lakini nyavu za kitambo na nira za kale hazitaweza. Lazima uunganishwe kwa nira ya yesu na uwe katika mtandao mpya maana kwa
nguvu zako hauwezi..

**NIRA YA KIFUNGO**

Zote tu katika nira ya aina moja au nyingine, aitha uwe katika nira ya Mungu
au nira ya kifungo Fulani..

Nira ya kifungo iko katika hali tatu , unaweza kuwa katika nira ya kifungo cha
kibinafsi, au dhabi, au mtu mwingine.

**NIRA YA DHABI:**

**Mimi ni Mungu wako niliekuleta kutoka inchi ya Misili (inchi ya dhabi) iliuondoke uache kuwa mtumwa wao, na nikavunja nira zako na kukufanya uwe huru. (Mambo ya Nyakati 26:13)**

Nira ya kimisili yamaanisha nira ya dhabi ambayo lazima iharibiwe ndani
yako.

**NIRA YA KIBINAFSI**

**Maana mambo yale ninayo taka kuyatenda siyatendi nayale nayatenda siyapendi…. (Warumi 7:15)**

Hali ya kunjipenda na malingo ni mifano ya nira za kibinafsi

**NIRA YA MWANADAMU:**

Hii ni nira ambayo wengine wamekuwekea katika maisha yako

**Maana wao huwawekea watu mizigo mizito mabegani mwao lakini wao hawaguzi hata kwa kindole kimonja (Matthew 23:4)**

Hali kam hitikandi za kindini, mipango na talatibu za kitamanduni na kadhalika.

**HALI TATU ZA NIRA YA MUNGU**
Nira ya Mungu ni kuhusu kazi ya pamonja na watu kufanya katika umoja sio
kuwekea wengine mizigo , ni nira ya pumziko sio ya uchovu ni nyepesi wala
sio nzito.kama tulivyo soma katika Matayo 11:28 )

**HATUA TATU ZA KUZIBA PENGO:**
Yesu alipeana hatua tatu za kuziba pengo hii ya nira.

**kunja:** Lazima unje kwake kwa hiali yako maana hii inavunja n**ira ya dhabi**

**Chukua:** Inakulazimu kuchukua nira yake, katika hayo basi nira ya mwanadamu itakuwa imeharibiwa.

**Njifunze naye:** Katika hali ya kunjifunza naye utakua umevunja nira ya kibinafsi maana atakunjaza.

**KUVUNJA NIRA**
Ni matumaini ya Mungu kwamba kila nira katika maisha yako ivunjwe iliupate kutimiza maono.
Wakati mmoja waisiraeli walizingirwa na njeshi la Ashuli na Bwana akanena
nao akisema;

**Bwana wa manjeshi ameapa na kusema, hakika kama nilivyokusundia ndivyo itakavyo kuwa, kwamba nitawavunja Waashuli katika shamba langu; na katika milima, na kumkanyangia chini ya miguu; na itakuwa kwamba nira yake itwaondokea na mizigo yake toka kwa mabega mwako (Isaiah 14:24-25)**
Bwana alitaka kuvunja nira kwa inchi ya waisiraeli pekee lakini hali hii iliendelea katika ulimwengu kote kama tunavyo ona katika Isaia 14:26 (tafadhali Soma)
Mipango ya Bwana ilikuwa kuvunja nira kwa watu wote wa mataifa ya ulimwengu ili wewe mwenyewe unjitwike nira yake. Kusundi ya Mungu ni
kukuondoa katika nira ya kira aina ili uweze kuwa katika nira yake.

**JE, NIRA ITAVUNJIKA ANJE?**
**...na nira itavunjika kwasababu ya mafuta (upako) (Isaiah 10:27)**
-Nira haitavunjika kwa sababu ya masomo au mambo mengine yeyote lakini
kwa sababu ya upako kupitia Roho wa Mungu si kwakusundi tu ya maisha
yako laki hata kwa sababu ya mataifa ya ulimwengu.baada ya Mungu

kuvunja nira katika maisha yako basi inakuhitanji upate kunjua kwamba
angependa kukutumia kuvunja nira za mataifa ya ulimwengu.kama ilivyo
andikwa katika Isaiya mlango wa 14:26-27. Soma tafadhali

**MATOKEO YA KUVUNJA NIRA**

Mungu akasema;

**Je, si hii ndio zaumu ninayo pendezwa nayo.. kufungua vivungo via uovu, kufungua mizigo ya waliobebeshwa… na kuvunja kila nira… ? (Isaiah 58:6)**

Baada ya hiyo akanakili matokeo ya kuvunja nira (Soma kuendelesha)

**Basi utaitana, na Bwana atakusikiliza, utalia na Bwana atasema mimi hapa (Isaiah 58:9-12)**

Matokeo ya kuvunja nira ni yafuatayo;

1. -Utatambua sauti ya Mungu, maana utamwita naye atanjibu "mimi hapa"(Mstari 9)
2. -Utanawili katika kuyatimiza maono yako, maana nuru yako itaangaza,
3. kumaanisha hali ya kunawili. (Mstari 10)
4. -Bwana atakuongoza milele. (Mstari 11)
5. -Atakuwa akigalimikia mahitanji yako. (Mstari 11)
6. -utaweza kuzaana. (Mstari 11-12)
7. -Utakuwa kama shamba linyunyuziao maji, na kuwa na faida katika ulimwengu wa kiasili na wano wako katika kiroho watanjenga upya manjengo ya kale katika mizingi sawa. .

Neti ya kitabo imevunjika na kushakaa, haifai kamwe, maana haiwezi kuyashukua mavuno mapya, ndivai mpya, kunjengewa msingi mipya kwa
sababu ni mawazo ya watu na mchanganyiko wa kitamanduni. Maono ya
mavuno ya kiroho itahidhilishwa na mtu mwenye upako unao weza kuvunja
nira za kila aina.

# MASWALI YA KUNJIPIMA

1. Andika mustali kielelezo bila kutazama popote.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Je, nira tatu ni zipi?

____________________ ____________________ ____________________

3. Andika maneno matatu yanayoeleza nira ya Mungu.

____________________ ____________________ ____________________

4. Je, nizipi hatua tatu ili uweze kuzimba pengo kati ya nira la utumwa na nira
ya Mungu?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

5. Andika matokeo tano baada ya kuvunja nira kama ilivyo andikwa katika
isaiya 58

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

(manjibu nyuma ya kitabu.)

# MAFUNZO YA ZIADA

Ni nira gani kati ya hizi zinakuzia kutenda kazi ya Mungu?

_____dhabi
_____ndini
_____uoga
_____kukosa uwezo
_____Shuku
_____nguvu zako
_____Mengine:_______________________________________

Soma andiko hii: Isaiah 14:24-27
Ndai ahadi hii: Isaiah 10:27
Omba ombi hili:
Bwana, asante kwa sababu ya maono ya mavuno ulioiweka ndani yangu,
Nakuomaba uvunje nira ya
----------------,-------------------,-----------------------na
ya ------------------ katika maisha yangu (tanja nira hizo)
Niunganishe katika nira ya Yesu, Unda mtandao mpya katika maisha yangu
itakayoleta mavuno mengi.
Nakushukuru sasa kwa sababu ya upako ambao umevunja kila nira ya kifungo.
Katika Njina la Yesu,
Amina.

# SURA YA KUMI

## KUBARIKI MATAIFA

MAKUSUDI:
Baada ya kumaliza sura hii utaweza.
Kutambua sifazakiroho za Ibrahimu zilizomwezesha kubariki mataifa
Kutambua kuwa wewe ni mrithi wa ahadi za Abrahamu
Kutambua jukumu lako kama mrithi kubariki mataifa ulimwengu

MSTARI WA KUKUMBUKA
"Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu na warithi sawasawa na ahadi" (Wagalatia 3:29)

UTANGULIZI
Ibrahimu alichaguliwa na Mungu kuwa baba wa mataifa. Kupitia yeye mataifa yoet ya ulimwengu yatabarikiwa
"Na katika uzao wake mataifa yote ya dunia watajibarikia kwa sababu umetii sauti yangu." (Mwanzo 22:18)
Agano jipya linajunua wazi jinsi ambavyo waamini wote ni warith wa ahadi ya Mungu aliyompa Ibrahimu. Kuwa mrithi maana yake ni kwamba umetithi toka kwake.
"Fahamuni basi ya kuwa, wale walio wa Imani, hao ndio wana wa Ibrahimu na andiko kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki mataifa kw imani lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani kusema katika wewe mataifa yote watabarikiwa, basi hao walio wa Imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye Imani.
Wewe ni mrithi kwa sababu umekuwa ni uzao wa Ibrahimu kupitia Yesu Kristo.
"Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu na warithi sawasawa na ahadi" (Wagalatia 3:29)
Kama wewe ni uzao wa Ibrahimu, wewe ni mrithi sawasawa na ahadi ya wokovu. Lakini kama wewe ni mrithi pia umepewa jukumu la kuwabarikia mataifa ya ulimwengu habari njema ya Injili. Umebarikiwa kudai urithi wako;

"Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako na miisho ya dunia kuwa milki yako" (Zaburi 2:8)
Kupitia Ibrahimu mataifa ya ulimwengu yatabarikiwa. Kupitia Yesu Kristo mataita pia ni urithi wako.

SIFA ZA KIROHO

Zifuatazo ni sifa za kiroho Ibrahimu alikuwa nazo zilimfanya awe baraka kwa mataifa, wa jinsi ambavyo hizi sifa zinavyohusiana na maono ya mavuno.

ALIKUWA AMESHAWISHIKA

Abrahamu aliamini maono ya Mungu ambayo amemwonyesha. Yesu alikuwa ameshawishika kiasi kupitia yeye Mungu atawabarikia mataifa ya ulimwengu.
"Huku akijua hakika Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi" (Warumi 4:21)
Kwa maono ya mavuno ili kuwa kila hasisi lazima ushawishike. Mungu ameahidi mavuno mengi ametoa mbinu na njia. Umeitwa kama mtendakazi kwa ajili ya kuwabarikia mataifa ya ulimwengu.

ALIWEKEZA KATIKA MAMBO YA KIROHO

Ibrahimu aliwekeza maisha yake yote katika kile ambacho kilikuwa hakionekani katika ulimwengu huu. Mungu alimpa Ibrahiimu ahadi ya nchi nzuri ambayo alikuwa hata hajaweka nguvu katika nchi hiyo;-
"Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka mguu, akaahidi kwamba atampa iwe milki yake na ya uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto."
(Matendo 7:5)
Nchi iliahidiwa ambayo Ibrahimu hajaiona iliahidiwa kwamtoto ambye alikuwa hana bado. Ibrahimu hakuwa na hofu juu ya Mungu. Akawekeza maisha yake katika mpango wa Mungu ili ahadi ya Mungu itimizwe kwa vizazi vijavyo. Maono ya mavuno kwa asili ni milele. Utachukua maisha yako yote ukiwekeza kwa vitu vile ambavyo havionekani, lakini matokeo ni milele. Vizazi vijavyo vitabarikiwa kwa sababu ya umetimiza maono.

ALIKUWA MTII KWA WITO

Ibrahimu alipitwa na Mungu kwenda sehemu ambayo baadaye atapokea urithi, alitii.

“Kwa imani Ibrahimu, alipoitwa kwenda katika nchi asiyoijua ili akapokee urithi hakusita katika kutii; na akaend, bila kujua anakokwenda” (Waebrania 11:8)
Haitoshi tu ukiitwa kwa ajili ya maono ya mavuno. Lazima uitike kwakutii wito
“Na uzao wako mataifa yote ya dunia yatajibarikia; kwasababu umeitii sauti yangu”(Mwanzo 22:18)

ALIKUWA TAYARI KUSIMAMA PEKEE
Mungu alizungumzia Ibrahimu
“Mwangalieni Ibrahimu baba yenu, na Sara mlikotokea; kwasababu nalimwita, nikambariki, na nikamwongeza” (Isaya 51:2)
Ibrahimu aliitwa peke yake ilibidi kuacha nyumba yake, familia yake, ili aitike wito. Unapoitwa na Mungu kuokoka ni jambo la kibinafsi. Kilamtu inabidi aitike binafsi kwa wito ule. Wito wa mashamba wa mvuno ni sawasawa. Kama Ibrahimu, umeitwa peke yako, lazima ufanye uamuzi wa kuacha nyumba, familia. Bila shaka itakubidi kutoka nje ya wale wasiohusika ambao bado hawajapata maono.

ALIKUWA NA MAONO YA KIROHO
Ibrahimu alikuwa na maono ya kiroho
“Kwasababu aliuangalia mji ambao misingi yake mjenzi na mhandisi wake ni Mungu”    (Waebrania 11:10)
Maono yake yalikuwa ni mambo ya kiroho.maono yke yalikuwa mji ambao mjenzi nia Mungu. Ikamfanya akae katika nchi mpya kwake, akakaa katika ahema tofauti na nyumbani na familia, maono yalibadilisha maisha yake.
Maono ya mavuno yamebadilisha maisha yako, hutakuwa kama ulivyo, hauwezi ukafanana na vitu vya muda vinavyopita. Unatafuta vitu vya milele.

ALIMJUA MUNGU VIZURI
Ibrahimu liitwa “rafiki wa Mungu” maandiko yale ya kutimizwa yaliyonena Ibrahimu alimwamwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki, naye aliitwa rafiki wa Mungu.
“Na andiko likatimia lililosema, Ibrahimu alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa ni haki: na akaitwa ni rafiki wa Mungu (Yakobo 2:23).

Kinatakiwa ni uhusiano wa kibinafsi na Mungu ili kutimiza maono. Lazima ujifunze njia zake na kuweza kusikia sauti yake. Unatakiwa uwe rafiki wa Mungu.

ALIKUWA AMEJAA TUMAINI

Paulo anazungumza juu ya Ibrahimu;
"Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa ili apate kuwa baba wa mataifa mengi kama ilivyonenwa ndivyo utakavyokuwa uzao wako." (Warumi 4:18)
Ingawa alikuwa hana mtoto, Ibrahimu alipokea ahadi ya baba wa mataifa mengi. Katika kawaida ilikuwa kukosa tumaini lakini ile sura ya kukosa tumaini Ibrahimu aliamini tumaini.
Haijalishi unakutana na mazingira gani, haijalishi tatizo lako linavunja tumaini kwa kiasi gani,
Fahamu kwamba Mungu amekuita katika maono ya mavuno na yatatimizwa tu. Kutna na kuvunjika tumaini pamoja na kuondoa shaka, "kile alichoahidi, ana uwezo wa kukifanya" (Warumi 4:21)

ALIKUWA NA IMANI YENYE NGUVU

"Lakini akiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini bali alitiwa nguvu kwa Imani akimtukuza Mungu." (Warumi 4:20)
Ibrahimu alikuwa na Imani ambayo ilimtukuza Mungu kwa kutimiza maono hata kabla hayajatokea alikuwa na hakika ya kufanya chochote alichoahidi. (Warumi 4:20)
Ukubwa wa maono ambayo Mungu amekuitia unatisha; watu bilioni tatu bado hawajapokea ujumbe wa Injili. Hawa ni wapagani waha ni urithi wako kupitia wewe watabarikiwa.
Usiyumbe katika ahadi za Mungu, usiangalie ukubwa wa kazi kabla yako, lakini angalia ukubwa wa Mungu. Mungu ameahidi mavuno mengi ya kiroho, uwe kama Ibrhimu ambaye "…………. Aliamini kwa kutarajiwa yasiyoweza kutarajia …………"
(Warumi 4:18 Biblia ya Living)

ALIKUWA NI MWENYE HAKI

Kwasababu Ibrahimu aliamini Mungu.
"Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki"(Warumi 4:22)

kama ulivyojifunza awali katika somo hili, msingi wa utendakazi wako katika mavuno lazima uwe ni haki.

ALIKUWA MPOLE

Paulo alisema, Ibrahimu alimpa utukufu Mungu. (Warumi 4:20). Ibrahimu jinsi ya kutimiza maono kupitia Mungu, yeye pekee Mungu, anastahili utukufu. Mungu amekupa maono makubwa katika shamba la maono wa mataifa ya ulimwengu. Lakini kutimiliza kunakuja kupitia yeye. Huwezi kupokea utukufu kwa ajili ya maono na matokeo ya kazi, utukufu lazima uende kwa Mungu kwa maono yaliyotimizwa.

ALIKUWA MWENYE KUTAKA AMANI

Katika Mwanzo 13 watumishi wa Lutu na Ibrahimu walishindwa kuelewana kuhusiana na haki ya maji, Ibrahimu alifika kwa ajili ya kutatua tatizo. Ujumbe wa kuzliwa kwa Yesu ambao ulileta na malaika ulikuwa ni Amani. Kwamba Injili ambayo unaipeleka kwa mataifa Injili ya amani pekee kupitia Mungu kuwa amani ya kweli itakuja.

ALIFANYA HARAKA KUFANYA MAPENZI YA MUNGU

Mungu aliposema na Ibahimu juu ya ahadi ya Agano katia yake na Mungu, ilikuwa ni kutahiriwa. Biblia inanukuu siku ileile Mungu liposema na Ibrahimu, Ibrahimu na watu wake wote wa nyumbani mwake walitahiriwa. (Mwanzo 17)
Wakati mwingine Mungu baadaye alitimiza ahadi yakekwa Ibrahimu na yeye pamoja na mkewe Sara walikuwa na mtoto wa kiume. Baada ya kuzaliwa Isaka, Mungu akampa Ibrahimu jaribio gumu sana. Akamwambia kutoa sadaka mtoto weke wa kiume katika (Mwanzo 22) Kupitia Isaka, kulikuwa na ahadi ya Mungu alikuwa mrithi kwa ukoo wa Ibrahimu ujao. Isaka ndiye lilipitia taifa la Israeli, kwalo ulimwengu wote utabarikiwa. Bado Mungu akamwambia Ibrahimu kumtoa mtoto wake wa kiume kuwa sadaka.
Biblia inaonyesha katika Mwanzo 22:3 kwamba Ibrahimu alipokea ujumbe toka kwa Mungu “Akaamka mapema asubuhi” ili kutii maagizo. Hata kama mapenzi ya Mungu ni magumu, Ibrahimu hakuchelewa. Mungu alipozungumza naye, alitenda hapohapo kwa haraka. Kutokanana kutii kwake, Mungu akatoa sadaka nyingine na maisha ya Isaka yakaokolewa. Mavuno katika mashamba ya mavuno hakiwezi kuwa kitu rahisi mpaka Mungu anapozungumza unatendea kazi. Unapoanza kuchukua hatua ya utii, Mungu atatenda upande wake Ibrahimu hakuona

kuwa agizo la Mungu kuhusiana na Isaka lilikuwa ni sadaka, yeye aliita ni "kuabudu".

Kuabudu kwa hali ya juu ni kuangalia zaidi ya Isaka ambaye ndiyo Mungu anapenda.

Mungu amekupa maono na yamebadilisha maisha yako na usifanye maono kuzidi uhusiano wako na Mungu. Jambo la muhimu ni kuwa na uhusiano na Mungu.

Munu alimjaribu Ibrahimu ili kuona kuwa Isaka ametawala maisha yake au Mungu. Lazima Mungu ndio awe anatawala maisha yake. Maono hayawezi kuchukua nafasi nafasi ya mtoa maono.

ALIKUWATAYARI KUONDIKA KWA AJILI YA MUNGU

Ibrahimu aliishi maisha rahisi sana ambayo yalimwezesha kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya Mungu. Alikuwa na uwezo kuondoka haraka kutii amri ya Mungu. Mwanzo 12.

HAKUANGALIA NYUMA

Ibrahimu hakuhitaji maisha ya zamani aliyoyaacha nyuma, yeye aliangalia sana maisha mapya na mambo mapya ambayo Mungu alimpanyia.

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu; kwa kuwa kila amwendeaye lazima aamini kuwa Mungu yupo, tena huwapa thawabu hao wamtafutao kwa bidii" (Waebrania 11:6)

ALITEMBEA KWA UFUNUO WA MAARIFA

Ibrahimu alitendea kazi ufunuo kutoka kwa Mungu badala ya kutoa sababu nyingi zisizo na msingi.

"Bwana akasema, je nimfiche Ibrahimu jambo nilifanyalo?" (Mwanzo 18:17)

HAKUANGALIA UWEZO WAKE BINAFSI

Ahadi za Mungu kwa mataifa akazaliwa mtu mmoja "kama mfu" kawaida Ibrahimu alikuwa hawezi kutimiza mpango wa Mungu.

"Na kwa ajili ya hayo, wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao na kama mchanga ulio ufueni, usioweza kuhesabika," (Waebrania 11:12)

ALIMTAFUTA MUNGU

Katika Mwanzo 12 inatuonyesha Ibrahimu akajenga madhabahu na akaliitia Jina la Bwana.

## ALIJISHUGHULISHA NA MAMBO YA WATU WENGINE

Soma habari ya Ibrahimu na Lutu katika Mwanzo 14 kama unataka kuwa "Mkristo hapa duniani" unatakiwa ujishughulishe na mahitaji ya wale wanaokuzunguka.

## ALIKUWA MKARIMU

Ibrahimu alitoa sehemu ya kumi ya chochote alichokuwa nacho.
"Ahimidiwe Mungu aliye juu sana aliyewatia adui zako mikononi wako. Ibrahimu akampa fungu la kumi la vitu vyote alivyokuwa navyo."
(Mwanzo 14:20)

## ALIKUWA TAYARI KUKAA KATIKA NCHI YA UGENI

Kwa imani alikaa ugenini, katika nchi ile ya ahadi, kama nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka ana Yakobo warithi pamoja katika ahadi ile. (Waebrania 11:9). Alikuwa tayari kuheshimu mila za desturi za wengine mfano kuinama mbele ya watu wa nchi ile ilikuwa ni mila na desturi.
"Ibrahimu akainama mbele ya watu wa nchi" (Mwanzo 23:12)

## ALIZALISHA WATU WANAOFANANA NAYE

Hii inaonyesha wazi katika maisha ya mtumishi wake Eliezeri (Mwanzo 24)

## ALITOA UTUKUFU KWA MUNGU

Mfalme wa Sodoma akamwambia Ibrahimu, Nipe mimi hao watu na hizo mali uchukue wewe. Ibrahimu akamwambia mfalme wa Sodoma, nimeinua mkono wangu kwa BWANA, Mungu aliye juu sana, Muumba wa Mbingu na nchi ya kuwa, sitatwaa uzi, wala gidamu ya kiatu, wala chochote kilicho chako, usije ukasema nimemtajisrisha Ibrahimu. Isipokuwa hivyo walivyokula vijana na sehemu za watu waliokwenda nami yaani Aneri, Eshkoli na Mamre na watwae hao sehemu zao. Kumbuka siku zote utukufu lazima uende kwa Mungu.

## MAONO YATIMIZWA

Ibrahimu, mtu mwenye maono ya kiroho. Alikuwa ni mtu ambaye kupitia yeye mataifa yatabarikiwa na maono yakatimizwa.

"Na kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi kama nyota za mbinguni wingi wao na kama mchanga ulio ufukoni usioweza kuhesabiwa." (Waebrania 11:12)
Wakati maono yalipotolewa kwa Ibrahimu. Wakati uliopita wa zamani ulikuwa hauzalishi na wakati huo ulikuwa hauzalishi. Lakini hakukubali kuwa mfu wa mwili na tumbo la Sara. Inawezekana mambo yako ya zamani yamekuwa hayazai kiroho. Na wakati wako wa sasa hauzalishi. Basi sasa umepokea maono ya mavuno kama Ibrahimu angalia kwa macho ya imani, akijua "yule ambaye ameahidi ana uwezo kufanya yote"

MASWALI YA KUJIPIMA

1. Andika mstari wa kukumbuka __________________
2. Andika mistari 2 yakuonyesha waamini ni marithi wa Ibrahimu na ______________
3. Sisi ni warithi wa ahadi ya_________________
4. Sisi ni wawili wa jukumu la _____________________
5. Andika sifa za kiroho za Ibrahimu zilizo mfanya kutimiza maono ya baraka kwa mataifa______ __________ _________ ____________ ________ _________

KWA KUJIFUNZA ZAIDI

Ifuatayo ni sehemu ya sifa za kiroho za Ibrahimu ambayo matokeo yake ni baraka kwa mataifa yote ya ulimwengu. Kama unataka kutimiza maono ya baraka kwa mataifa unatakiwa uendeleze sifa za kiroho zinazofanana katika maisha yako. Itafakari kila sifa ya kiroho ya____
Eleza jinsi ambayo sifa hizi una hakika katika maisha yako kwako binafsi

| Sifa | Kwa kiwango gani ambayo sifa hizi zina uhakika Katika maisha yangu binafsi. |
|---|---|
| Umeshawishika kikamilifu | ________________________ |
| Umewekeza katika vitu vya kiroho | ________________________ |
| Utii | ________________________ |
| Uko tayari kusimama peke yako | ________________________ |
| Maono ya kiroho | ________________________ |
| Kumjua Mungu vizuri | ________________________ |
| Tumaini | ________________________ |

Imani ________________________
Haki ________________________
Unyenyekevu ________________________
Amani ________________________
Utayari kufanya mapenzi ya Mungu________________________
Kukubali kuhama kwa ajili ya Mungu ______________________
Kuotangalia nyuma ________________________
Kutembea katika ufunuo wa maarifa_______________________
Kutoangalia uwezo binafsi ________________________
Kumtafuta Mungu ________________________
Kupokea makukumu ya wengine ________________________
Ukarimu ________________________
Kuzalisha watu wanaofanana naye katika kujitoa _____________
Kutoa utukufu kwa Mungu ________________________
Kuwa tayari kukaa katika nchi ya ugenini ___________________

Kutokana na mchanganuo huu, utachukua hatua gani kuhusiana na maeneo yafuatayo ya kuendeleza sifa za kiroho ambazo unakosa

Usomaji wangu wa Biblia kila siku __________________
Maisha yangu ya maombi kila siku __________________
Nyumba yangu na familia __________________
Kanisa langu __________________
Mipango yangu kwa ajili ya baadaye __________________
Mipango yangu kwa ajili ya baadaye __________________
Kujihusisha kwangu na maono ya mavuno __________________
Fedha zangu __________________

# SURA YA KUMI NA MOJA

MAONO SASA YANAKUWA KITU HALISI

MAKUSUDI:

- Baada ya kumaliza somo hili utaweza;
- Kutambua watu ambao wameitwa kwa ajili ya mavuno
- Kudai ahadi ya Mungu ya mavuno mengi
- Kuyaweka maono kuwa kitu halisi katika maisha yako

Mstari Wa Kukumbuka:
“Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia moyo.”(Wagalatia 6:9)

UTANGULIZI
Ulipoanza kozi hii ulianza na uzoefu ambao utakuongoza kuokamaono hadi kwenye kitu halisi.
Kutoka kuzaliwa kwa maono ya mavuno, umeona ulimwengu kupitia macho ya Mungu na kuelewa makusudi kwa mataifa ya hapa ulimwenguni. Umejifunza vitu ambavyo vinazuia mavuno na mbinu, njia za zana kwa ajili ya mavuno mazuri. Umekwisha vunja Nira ya utumwa na desturi na kupokea uzoefu mpya wa nguvu ya Mungu.
Katika sura hii ya mwisho maono yanakuwa kitu halisi unapokuwasehemu ya kutimiza maono.

AKINA NANI MUNGU ANAWATUMIA
Akina nani huwa wanatumiwa kutimiza maono ya mavuno? Mtu aina gani baba au mama ambaye hutumika kuendeleza maono kupeleka Injili kutoka sehemu moja hadi nyingine?
Soma Marko sura ya 16 katika Biblia. Sura hii inakupa majibu ya maswali kwa maswali haya. Katika sura hii tunaona wanawake ambao wafuasi wa Yesu wakienda kaburini kuupaka mwili wa Yesu mafuta. Walipowasili walikuta……………
“Wakaingia kaburini wkaona kijana ameketi upande wa kuume amevaa vazi jeupe, wakastaajabu naye akawaambia msistaajabu, mnamtafuta

Yesu Mnazareti aliyesulubiwa, amefufuka hayupo hapa. Patazameni mahali walipomweka.
Wanawake walikwenda kuwashirikisha habari njema pamoja na wanafunzi. Ingawa Yesu alionekanakatika hali ya kuonekana mwili. Wanafunzi hawakuamini ya kuwa amefufuka." (Marko 16:11)
"Hatimaye Yesu akawatokea wale wanafunzi wawili walipokuwa wakitembea katika nchi."
Walipowaambia wenzao, hawakuamini. Mwishoni Yesu akawatokea wanafunzi.
"Baada ya Yesu kuongea nao kwa kutokuamini kwao, alisema; enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15)
Hakika atakuwa amefanya makosa. Hawa ni watu ambao walikwenda kuupaka mwili wa Yesu mafuta na baadaye kusheherekea ufufuo. Hao ndio watu ambao walilala wakati alipopata matatizo. Walimkana na walimakana na walijificha kutokana na hofu. Yesu alitumia miaka mitatu akawatayarisha watu kwa ajili ya kifo chake na ufufuo lakini bado wakimkataa wakati wa matatizo na walikataa kuamini juu ya ripoti ya kufufuka kwake. Dakika moja Yesu anawasahihisha kwa kutokuamini kwao. Na anawapa changamoto na maono ya mavuno ya kiroho katika mashamba ya mavuno katika mataifa duniani. Jinsi gani iliwezekana kuacha mambo ya mbele ya Injili katika mikono ya wanafunzi hao? Kwa sababu alikuwa hawaangalii kama walivyo. Alikuwa haangalii mambo ya nyuma, au hali ya sasa. Aliwaona kuwa wataweza wakipewa msaada wa Roho Mtakatifu.
Mungu hatafuti mambo yako ya zamani kusindwa kwako, wasiwasi wako, au kutokuamini kwako. Yeye anaangalia kile anachofahamu unaweza kuwakwa msaada ya Roho Mtakatifu.

WATU AMBAO MUNGU ANAWATUMIA
Hebu tuone katika historia watu ambao Mungu amewatumia kutimiza makusudi yake.

YAKOBO
Mungu ilibidi achague Yakobo mtu ambaye alihitaji sana haki ya mzaliwa wa kwanza. Ilimbidi adanganye kwa hilo na Esau ambaye hakuchukulia umuhimu akaiuza kwa bakuli ya supu. Bado alitumiwa Yakobo kwa ajili ya taifa la Israeli.

IBRAHIMU

Yeye ni baba wa mataifa mengi. Alipopokea ufunuuo huo toka kw Mungu alikuwa mwenye uso wake wa kucheka kwa kutokuamini. (Mwanzo 17:1 – 3). Baadaye huyu mtu wa imani akadangaya adui akasema Sara ni dada yake kwa sababu alihofu maisha yake. Pamoja na yote aliitwa “Rafiki wa Mungu” na akawa baba wa mataifa mengi.

MUSA
Kutokutii kwake kumemfanya akae nje ya nchi ya ahadi bado aliwaokoa watu milioni 2 katika utumwa kule Misri na kuwaongoza jangwani kulingana na mpango wa Mungu.

DAUDI
Alichukua mke wamtu na akamuua mume wake ili kuficha ile dhambi bado aliitwa “mtu apendezaye moyo wa Mungu”, na Mungu akampa ufalme.

GIDEONI
Alikuwa akivuna ngano na kuficha kw hofu ya maadui wakati Mungu akimwita awakomboe wana wa Israeli. (Waamuzi 6)

WATU WA KAWAIDA KABISA
Mungu anawatumia watu wa kawaida kutimiza mapenza mapenzi yake. Yesu alipofanya muujiza wa kugeuza maji kuwa divai, akawaambia watu wa kawaida kujaza mabalasi maji. Wakati alipowaongeza samaki na mikate akawapa watu wa kawaida halafu wakawalisha kusanyiko la watu.
Wakati huo Yesu alipofanya muujiza mkubwa katika huduma yake ulikuwa ule wa kumfufua Lazaro katika kifo, aliwategemea watu wa kawaida kuondoa jiwe katika mlango wa kuingia kaburini. Je Mungu huyohuyo aliyemfufua Lazaro hanayo nguvu ya kuondoa jiwe kutoka katika mlango w kuingia kaburini?
Ndivyo Mungu amekuwa akiwatumia watu kutimiza mpango wake; njia zake ni watu. Mungu anawaita watu wa kawaida na kuwafanya kuwa zaidi ya kawaida. Yeye anawainua watu kutoka uwa wasikilizaji na kuwa washiriki katika mpango wake.
Watu wanaofikiria wa kawaida wanaofikiria kuwa hawawezi kutumiwa na Mungu.
Wewe mu wa kawaida unayefikiria hawawezi kuwa sehemu ya muujiza…………..
Wote waliokmkana na kumwacha…………

Mungu haangalii mambo yako ya nyuma au utendaji wako wa sasa. Hakuangalii kama unavyojiangalia. Anakuangalia wewe kama utakayepokea changamoto na kwenda kwenye shamba la mavuno, ulimwenguni. Anakuangalia wewe jinsi utakavyokuwa baada ya kujazwa na nguvu zake.
Mungu hategemei imani yako, elimu, vipawa au kiwango chako cha elimu au cha kiroho. Hategemei kitu chochote au jinsi ulivyo. Anategemea kitu anachojua yeye kwamb atakuwa kama utayatoa maisha yako yote kwa mapenzi yake na kusudi lake.
Ulimwengu wa kanis lakwanza haukufikiwa na wahubiri wakubwa, ulifikiwa na watu wa kike na kiume ambao waligeuza macho yao katika kwao wenyewe, kushindwa kwao na wakakamata maono ya mavuno. Wakagundua kwamba wakati wao ni dhaifu kimwili wako na nguvu kiroho. Mungu ameahidi;
"Neema yangu yakutosha; maana uweza wa Mungu hutimilika katika udhaifu."
(2Wakorintho 12:9)

MAVUNO MENGI
Kwa wote wanaokamata maono na kutimiza kazi na mapenzi ya Mungu, kuna ahadi ya mavuno tele;
"Kwa maana itakuwepo mbegu ya amani; mzabibu utatoa matunda yake, nayo ardhi itatoa mazao yake na hizo mbingu zitatoa umande wake; nami nitawarithisha mabaki ya watu hawa vitu hivi vyote." (Zekaria 8:12)
atageuza jangwa kuwa shamba lenye rutuba.
"Amegeuza jangwa ikawa ziwa la maji, na nchi kavu ikawa chemchemi za maji.
36 Maana amewakalisha huko wenye njaa, nao wametengeneza mji wa kukaa.
37 Wakapanda mbegu katika mashamba, na kutia mizabibu iliyotoa matunda yake" (Zaburi 107:35 – 37)
Mungu ataleta mavuno kwa maeneo yenye kuzaa kwa hafifu;
"Na uwepo wingi wa nafaka katika ardhi ya milima; matunda yake na yawayewaye kama Lebanoni, Na watu wa mjini wastawi kama majani ya nchi" (Zaburi 72:16)
Umri sio kikwazo kwa mpango wake
"Utazaa matunda hadi wakati wa uzee" (Zaburi 92:14)
Unaweza kwenda unalia kwa uchungu hadi kuzaliwa kwa maono lakini …….

“Wapandao kwa machozi, watavuna kwa kelele za furaha, ingawa mtu anakwenda zake akilia azichukuapo mbegu za kupanda……” (Zaburi 126:5 – 6)
Huwezi kuelewa wingi wa mavuno wakati huu wa mwisho.
“Je, mbegu ingali ghalani? Naam huo mzabibu , wala mtini, wala mkomamanga, wla mzeituni haukuzaa kitu tangu siku hii ya leo nitawabariki” (Hagai 2:19)
Mungu anaposema mavuno ni mengi, hii inaendelea kuwa hivyohivyo.
“Angalieni siku zinakuja asema BWANA ambazo huyo alimaye atamfikilia avunaye na yeye apandaye mbegu, nayo milima itadondoza divai tamu na vilima vyote vitayeyuka.” (Amos 9:13)
Utakuwa kabla ya kumaliza kupukuchua mavuno mpaka mavuno mengine ya kujie. Ndio maana hitaji la watenda kazi ni la haraka. Alimaye anamshinda avunaye. Maono ya mavuno yako mbele yako.
Dai ahadi ya mavuno mengi
Dai wapagani, mataifa kuwa urithi wako.
Mashamba ya ulimwengu yako mbele yako, inua macho yako na utazame.

MAVUNO YA MWISHO
Itakuja siku ya mwisho wakati Mungu atawaamuru malaika zake.
“Na malaika mwingine akatoka katika hekalu akimlilia kwa sauti kuu yeye aliyekuw ameketi juu ya lile wingu, tia mundu wako ukavune; kwa kuwa sa ya kuvuna imejuja kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa.” (Ufunuo 14:15) Katika ulimwengu mlolongo utakuja kutoka bara la Afrika, Bara la Ausralia, Bara la Ulaya, Bara la Amerika Kaskazini na Kusini, Bara la Asia na Visiwa vyote vya bahari………….. wavunaji wanatiririka kuelekea katika kiti cha Enzi cha Mungu.
Akina baba na mama ambao wamefanya maono kuwa halisi …………… wale ambao wameishi na maono kufanya jambo la msingi, wale ambao wamefufa wakiwa wamezibeba zile ahadi watapoleta mavuno ya dunia.
“Kisha nikaona, na tazama mkutano mkubwa ambao hapana awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, watoto, kwa wakubwa, watu wa kila kabila wamesimama mbele ya kiti cha enzi mbele za Mwana kondoo alievikwa vazi jeupe akiwa na tawi la mtende mkononi mwake. Wakalia kwa sauti kuu wakisema, wokovu una Mungu wetu aketiye kwenye kiti cha enzi na Mwanakondoo ………….. wakaanguka mbele ya kiti cha enzi wakimwabudu Mungu sura zao zikielekea chini.

Wakisema, Amina: Baraka na Utukufu na Hekima na Shukrani na Heshima na Uweza na Nguvu zina Mungu wetu milele na milele. Amina (Ufunuo 7:9 – 12)

JARIBIO BINAFSI

1. Andika Mstari wa kukumbuka ___________________
2. Andika nukulu tatu za Biblia zinazoahidi mavuno tele ________________
3. Wataje watu watano tuliowaongelea katika sura hii ambao Mungu aliwatumia bila kujali madhaifu yao ______________________
4. Mstari gani unaotueleza mavuno ya mwisho duniani yatakayofanywa na malaika wa Mungu ______________________

# MAJIBU KWA MAJARIBIO BINAFSI

SURA YA KWANZA

1. "Pasipo Maono, watu huacha kujizuia" (Mithali 29:18)
2. Maono ya kiroho yanahusika kuona zaidi ya ulimwengu wa kawaida katika ulimwengu wa kiroho. Ni kuelewa makusudi ya kimungu na kugundua sehemu ya mpango wake. Ni taswira halisi ya mambo ambayo Mungu anataka kutueleza kila hatua kwa kila Mkristo ili kufikia lengo.
3. 2,3,1,4,6,5
4. 3,1,4,2

SURA YA PILI

1. "Hamsemi ninyi Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari mavuno" (Yohana 4:35)
2. Ukiongelea asili sambamba na kiroho maana yake Mungu anatumia vitu vya asili kama mfano wa kuelezea kweli ya kiroho.
3. Mfano ulikuwa mavuno
4. Konde ni ulimwengu Mathayo 13:38
5. Unaweza ukazitaja sababu zifuatazo. Mavuno ni mfano ambao waafunzi wangeweza kuelwa vizuri
6. Uchumi wa Israeli ulikuwa katika kilimo
7. Sikukuu za kidini zilizunguka kimavuno.
8. Mavuno ilikuwa shughuli ya mwaka mzima
9. Kuna kanuni za kiasili za kupanda na kuvuna zinazuweza kutumiwa katika mavuno.
10. Wanafunzi walitambua kwa haraka mifano ya mavuno
11. Hamsemi ninyi: Usemi tu juu ya mavuno
12. Miezi minne tayari: Hamjachelewa
13. Mimi nawaambia: Sikiliza vile Yesu anasema
14. Inueni macho yenu: geuzeni kutoka kutokuona vema
15. Angalieni mashamba: oneni ulimwengu kwa macho ya Mungu.

SURA YA TATU

1. Macho yake kwa mataifa (Zaburi 66:7)
2. Kwa makadirio kama bilioni tatu.
3. Kama bilioni lugha.
4. Kuona ulimwengu kama shauri la mavuno linahitaji watendakazi
5. Dhambi
6. A.F b.F c. T
7. Ulimwengu wa Kikristo ni ndivyo anavyo hesabu kila siku kwa ajili ya kazi kuu, hasa kwa wasiofikiwa na Injili.

SURA YA NNE

1. 1."Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. [10] yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia, naam katika yeye huyo." (Waefeso 1:9 – 10)
2. 2. A.F a.T c. T d.T
3. Jibu lako lihusishe sehemu angalau zifuatazo mpango wa Mungu tangu mwanzo wa uumbaji ni kuweka vitu vyote vya mbinguni na duniani chini ya Yesu Kristo.
4. (Waefeso 1:9 – 10). Hapendi mtu yeyote apotee bali kila mtu katika kila taifa atubu na kumjua Kristo" (2Petro 3:9)

SURA YA TANO

1. "Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwakuwa apandacho mtu, ndicho atakachovuna. [8] Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa roho, katika roho atavuna uzima wa milele." (Wagalatia 6:7 – 8)
   1. A.T b.F c.F d.F e.T f.T g.T
   2. Uadui, Uovu, Magomvi na Mwili
   3. Watu waliokombolewa wakiisha maisha ya kukombolewa.
   4. Isaya 16:10 au Yoeli 1:10 – 12, 16
   5. Yoeli 1:13 – 14; 2:12 – 13
   6. Marudio ya vichwa katika sura hii
   7. Kutokutii Neno la Mungu — Kuangalia mazingira
   8. Kumsahau Mungu — Nguvu zisizoelekezwa
   9. Kupanda kusiko sahihi — Magonjwa na wadudu
   10. Kutokuwajibika — Kuna kusiko sahihi
   11. Juhudi Binafsi — Ardhi isiyokwatuliwa
   12. Laana inayojiendeleza — Msingi usio haki
   13. Watendakazi wachache

SURA YA SITA

1. 1. "Wapandao kwa machozi, watavuna kwa kelele za furaha. [6] Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda, hakika atarudi kwa kelele za furaha aichukuapo miganda yake." (Zaburi 126:5 – 6)
   2. Mbinu ni kanuni, mjia au mipango ya kuifwata ili kulifikia lengo fulani.
   3. Kama ukikosa moja kati ya mbinu hizi, pitia vichwa vya habari vya sura husika
   4. Mti wa kwanza unaozalisha
   5. Kupanda ni muhimu ili kuvuna
   6. Hauwezi kuvuna katika msimu huohuo unaopanda
   7. Unavuna ulichopanda
   8. Ni lazima upande bila kujali hali zinazozunguka
   9. Mavuna ni sawa sawa na kiwangu cha kiasi ulichopanda
   10. Unaweza ukapanda mahali ambapo hautavuna na kuvuna mahali ambapo haujapanda
   11. Utavuna kama wewe ni mwaminifu
   12. Ili kuzalisha, mbegu ni lazima ife.

SURA YA SABA

1. "Maana kama nchi itoavyo machipuko yake, na kama bustani ioteshavyo vitu vilivyopandwa ndani yake; ndivyo Bwana MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote" (Isaya 61:11)
2. Mbegu inayoinayokua inakubaliana na mazingira fulani.
3. Kama ukikosa yoyote katika hali hizi za kukua kiroho, pitia katika vichwa vya habari katika sura husika: Maisha; Udongo sahihi; Maji: hewa: Nafasi: Mfumo wa mizizi: Kupumzika: Kujishikamanisha na mzabibu; Kukatiwa majani; Hali ya Hewa.

SURA YA NANE

1. "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika Uyahudi wote, na hata mwisho wa nchi."   (Matendo 1:8)

2 Timotheo 2:2

Nguvu

Gundua kuwa ni ya leo. Gundua chanzo; Kubali majukumu ya kibinafsi na katika kanisa.

SURA YA TISA

1. "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. [29] Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; [30] kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi." (Mathayo 11:28 – 30)
2. Dhambi, Ubinafsi, Wanadamu.
3. Nyepesi, Laini, Kupumzisha
4. Uje kwake, uchukue Nira yake, na Ujifunze kwake.
5. Utajua sauti ya Mungu; Utafanikiwa na kutimiza maono yako; Mungu atakulinda moja kwa moja; Atakuwa mfadhili wako; Utazaa matunda.

SURA YA KUMI

1. "Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu na warithi sawasawa na ahadi" (Wagalatia 3:29)
2. Wagalatia 3:10 na Wagalatia 3:29
3. Wokovu
4. Kubariki Mataifa ya Ulimwengu

| | |
|---|---|
| 5. Alihakikishwa kikamilifu | Matumaini Makuu |
| 6. Aliwekeza katika vitu vya rohoni | Shujaa wa Imani |
| 7. Aliitikia mwito | Haki |
| 8. Alikubali kusimama peke yake | Mnyenyekevu |
| 9. Mtu wa Maono | Mtu wa Amani |
| 10. Alimjua vizuri Mungu | Alijitoa kufanya mapenzi yake |
| 11. Aliondoka kwa ajili ya Mungu | Hakuangalia nyuma |
| 12. Alitembea kwa uUfunuo wa maarifa | Alimfikiria Mungu |
| 13. Alifikiria majukumu kwa wengine | Mtoaji |
| 14. Alitoa watu waliojitoa | Alitoa Utukufu kwa Mungu |
| 15. Hakuangalia uwezo wake mwenyewe | |
| 16. Alijitoa kukaa katika nchi ya ugeni | |

SURA YA KUMI NA MOJA

1. “Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia moyo.”(Wagalatia 6:9)
2. Unaweza ukatumia nukulu zifuatazo: Zaburi 72:16; Zaburi 92:4; Zaburi 107:33 – 37 Zaburi 126:5 – 6; Amosi 9:13; Hagai 2:19; Zekaria 8:12
3. Yakobo, Ibrahimu, Musa, Daudi, Gidioni.
4. Ufunuo 14:15